# NITAKUPENDA

*Emmanuel John Mrina*
*0755219491*
*Parokia ya Legho-Moshi*



**2.Sogea Sophia wangu, joto lako nisikie,**
**Sina shoka wala rungu, huzuni nikupatie,**
**Waache wenye majungu, furaha tujipatie,**
**Sophia mpenzi wangu, nitakupenda milele.**

**3.Karibu kusitawisha, penzi liwe la mvuto,**
**Uwe wangu wa maisha, nifunze kama mtoto,**
**Na kamwe sitakuchosha, sogea unipe joto,**
**Sophia mpenzi wangu, nitakupenda milele.**

**4.Ukae kwangu enzini, lala sinzia ridhika,**
**Tulia nikwite hani, uwe wangu malaika,**
**Nikubebe mgongoni, chini nisije kuweka,**
**Sophia mpenzi wangu, nitakupenda milele.**

**Kibwagizo:**




**NB:**
***Kibwagizo kitaunganishwa na kiitikio pia kabla ya shairi na baada ya shairi kuna pumziko.**
***Ruksa kutumia jina tofauti kulingana na uhitaji.**

**Maalumu kwa ajili ya Kaka Benjamini Julius na Sophia John wa Parokia ya Mt.Maliseli - Koromije Mwanza.**
**Mungu aisimamie ndoa yenu.**